# KATIBA YA CHAMA CHA UKOMBOZI WA UMMA

## (CHAUMMA)YA MWAKA 2012

## TOLEO LA PILI 2015

**YALIYOMO** **UKURASA**

UTANGULIZI………………………………….................................v

SURA YA KWANZA

1.1. JINA LA CHAMA…………………………………………………1

1.2. MAKAO MAKUU YA CHAMA …………………………………………..1

1.3. KATIBA ………………………………………………………………….1

1.4. BENDE YA CHAMA ……………………………………………………1

1.5. NEMBO YA CHAMA …………………………………………………...1

1.6. ITIKADI YETU NI DEMOKRASIA YA KIJAMII…………………………1

1.7. LUGHA RASMI ……………………………………………………………..1

1.8. FALSAFA YA CHAMA ………………………………………………….....1

**SURA YA PILI**

2.0. MALENGO NA MADHUMUNI YA MISINGI YA KISIASA YA CHAMA………2

2.1. MALENGO YA CHAMA NI KAMA IFUATAVYO ……………………………….2

2.2. MADHUMUNI YA CHAMA ……………………………………………………..2

**SURA YA TATU**

3.0. UANACHAMA ……………………………………………………………………3

3.1. KUJIUNGA NA CHAMA …………………………………………………………3

3.2. HAKI ZA MWANACHAMA ………………………………………………………4

3.3. WAJIBU WA MWANACHAMA …………………………………………………..4

3.4. KUONDOKA KATIKA CHAMA ……………………………………………......5

**SURA YA NNE**

4.0. UONGOZI KATIKA CHAMA ……………………………………………………..6

4.1. SIFA ZA KIONGOZI ……………………………………………………………..6

4.2. KUACHA UONGOZI ……………………………………………………………..6

**SURA YA TANO**

5.0. NGAZI NA VIKAO VYA CHAMA …………………………………………………7

5.1. MUUNDO WA NGAZI NA VIKAO VYA CHAMA …………………………………..7

5.2. NGAZI YA CHEMCHEMI ………………………………………………………………7

5.3. WAJUMBE WA MKUTANO WA CHEMICHEMI ……………………………………..7

5.3. KAZI ZA MKUTANO WA CHEMCHEMI ………………………………………………7

5.4. KAZI YA MWENYEKITI WA CHEMCHEMI……………………………………………8

5.5. KAZI ZA KATIBU WA CHEMCHEMI …………………………………………………..8

5.6. NGAZI YA TAWI ……………………………………………………………………………..8

5.6.2. WAJUMBE WA MKUTANO WA TAWI ………………………………………………….8

5.6.3. KAZI ZA MKUTANO MKUU WA TAWI ………………………………………………….9

5.6.4. KAMATI TA UTENDAJI WATAWI ………………………………………………………11

5.6.5. KAZI ZA KAMATI YA UTENDAJI WA TAWI …………………………………………..12

5.6.6. WAJUMBE WA SECRETARIATI

……………………………………………………………………12

5.6.7. KAZI ZA SECRETARIATI



3

……………………………………………………………………13
5.6.10. KAZI ZA MWEKA HAZINA WA TAWI
…………………………………………………..13
5.6.11.KAZI ZA AFISA HABARI NA TAARIFA KWA UMMA ………………………13
5. 7.NGAZI YA KATA/WADI ……………..……………………………………...14
5.7.1. VIKAO VYA KATA ……………………………………………………………14
5.7.2. WAJUMBE MKUTANO MKUU KATA ……………………………………..14
5.7.4. KAMATI YA UTENDAJI YA KATA ……………………………………………16
5.7.5. KAZI ZA KAMATI YA UTENDAJI YA KATA…………………………………17
5.7.6. WAJUMBE WA SEKRETARIATI YA KATA ………………………………...18
5.7.7. KAZI YA SEKRETARIATI YA KATA ……………………………………………18
5.7.8. KAZI ZA MWENYEKITI WA KATA ………………………………..………18
5.7.9. KAZI ZA KATIBU WA KATA/WADI …………………………….…………...18
5.7.10. KAZI ZA MWEKA HAZINA WA KATA ……………………………………..19
5.7.11. KAZI ZA AFISA HABARI NA TAARIFA KWA UMMA WA KATA …………………19
5.8. NGAZI YA JIMBO ………………………………………………………………………..19
5.8.2. WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA JIMBO………………………………………19
5.8.3. KAZI ZA MKUTANO MKUU WA JIMBO……………………………………………...20
5.8.4. KAMATI YA UTENDAJI YA JIMBO
…………………………………………………...22
5.8.5. KAZI ZA KAMATI ZA UTENDAJI WA JIMBO
………………………………………..22
5.8.6. SEKRETARIATI YA JIMBO …………………………………………………………..23
5.8.7. KAZI ZA SEKRETARIATI YA JIMBO ……………………………………………….24
5.8.8. KAZI ZA MWENYEKITI WA JIMBO …………………………………………………24
5.8.9. KAZI ZA KATIBU WA JIMBO ………………………………………………………..24
5.8.10. KAZI ZA MWEKA HAZINA …………………………………………………………..25



4

5.8.11. KAZI ZA HAFISA HABARI NA TAARIFA KWA UMMA WA JIMBO ………………25

5.9. NGAZI YA MKOA ………………………………………………………………..25

5.9.2. WAJUMBE WA MKUTANO WA MKOA …………………………………………….25

5.9.3. KAZI ZA MKUTANO MKUU WA MKOA ……………………………………………26

5.9.4. KAMATI YA UTENDAJI YA MKOA …………………………………………………28

5.9.5. KAZI ZAKAMATI YA UTENDAJI YA MKOA ………………………………………….29

5.9.6. WAJUMBE WA SEKRETARIATI YA MKOA ……………………………………..29

5.9.7. KAZI ZA SEKRETARIATI YA MKOA ……………………………………………..30

5.9.8. KAZI ZA MWENEKITI WA MKOA ………………………………………………..30

5.9.9. KAZI ZA KATIBU WA MKOA ……………………………………………………..30

5.9.10. KAZI ZA MWEKA HAZINA WA MKOA ……………………………………………….30

5.9.11. KAZI ZA AFISA HABARINA TAARIFA KWA UMMA WA MKOA ………………….30

5.10. NGAZI YA TAIFA……………………………………………………………………36

5.11. WAJUMBE WA MKUTANO MKUU TAIFA…………………………………………...36

5.12. KAZI ZA MKUTANO MKUU WA TAIFA……………………………………………..37

5.13. WAJUMBE WA HALMASHAURI KUU YA TAIFA……………………………………..38

5.14. KAZI ZA HALMASHAURIKUU TAIFA………………………………………….......40

5.15. KAMATI KUU YA HALMASHAURI KUU……………………………………………..41

5.16. KAZI ZA KAMATI KUU YA HALMASHAURI KUU YA TAIFA……………………. …41

5.17. SEKRETARIATI YA KAMATI KUU……………………………………………………43

5.18. KAZI ZA SEKRETARIATI YA KAMATI KUU YA TAIFA………………………………44

**SURA YA SITA**

6. MUUNDO WA NGOME ZA CHAMA……………………………………………..45

6.1. NGOME YA WAZEE…………………………………………………………………45

6.2. NGOME YAWANAWAKE……………………………………………………………45



5

6.3. NGOME YA VIJANA……………………………………………………………………….45
6.4. NGOME ZOTE ZA CHAMA YATAKUWA CHINI YA UONGOZI WA CHAMA WA NGAZI HUSIKA NA…………………………………………………………………………45
6.5. MASHARTI YA KUWA MWANACHAMA WA KILA NGOME………………………45
6.6. KANUNI ZA KUENDESHA NGOME NA UCHAGUZI NDANI YA NGOME….45

**SURA YA SABA**

7. BARAZA LA WADHAMINI LA CHAMA…………………………………………………46
7.1. MWENYEKITI WA BARAZA…………………………………………………………46
7.2. KATIBU WA BARAZA………………………………………………………………….46
7.3. WAJUMBE SITA; WAKIWEMO WALAU WANAWAKE WAWILI…………………….46
7.4. MAJUKUMU YA BARAZA LA WADHAMINI………………………………………..46

**SURA YA NANE**



8. VIONGOZI WAKUU WA CHAMA NA KAZI ZAO…………………………………………47
8.9. MWENYEKITI WA TAIFA……………………………………………………………….48
8.10. MAKAMU MWENYEKITI WA TAIFA…………………………………………….....49
8.11. KATIBU MKUU……………………………………………………………….........49
8.12. NAIBU MAKATIBU WAKUU………………………………………………………….50
8.13. MUWEKA HAZINA WA CHAMA WA TAIFA……………………………………..50

**SURA YA TISA**

9.1. MASHARTI KUHUSU MGOMBEA URAIS……………………………………………….50

**SURA YA KUMI**

10. MAMBO YA JUMLA NA MUHIMU KUHUSU CHAMA…………………………………51

10.1. UCHAGUZI……………………………………………………………………………51

10.2. RUZUKU NA MAPATO MENGINE YA CHAMA……………………………………..52

10.3 AKIDI YA KILA KIKAO CHA CHAMA…………………………………………………52

10.4. UITISHAJI WA KIKAO……………………………………………………………….52

10.5. MJUMBE WA KIKAO KUPOTEZA SIFA……………………………………………..53

10.6. RATIBA YA VIKAO…………………………………………………………………..53

10.8. KUKASIMU MAMLAKA NA MADARAKA……………………………………………53

10.9. KUKAIMU MADARAKA……………………………………………………………..54

10.10. KURA ZA UAMUZI………………………………………………………………….54

10.11. KAMATI YA NIDHAMU, USULUHISHI NA MAONYO…………………………….54

10.12. TAASISI, ASASI NA NISHANI ZA CHAMA………………………………………….54

10.13. MABADILIKO/ MAREKEBISHO YA KATIBA……………………………………55

10.14. CHAMA KUUNGANA NA CHAMA KINGINE/VYAMA VINGINE VYA SIASA…. 55



*7*

# UTANGULIZI

## NA KWA KUWA;

Sisi wanachama wa chama cha UKOMBOZI WA UMMA (CHAUMMA)ni waumini wa Demokrasia ya kijamii tukiamini katika misingi ya demokrasia pana kwa jamii pana inayozingatia ujenzi wa jamii huru inayoheshimu haki za binadamu na ustawi katika misingi na falsafa ya usawa kwa binadamu wote.
Tunapigania ujenzi wa jamii isiyo na ubaguzi wa aina yoyote kwa misingi ya rangi, jinsia, asili, wala dini.
Sisi wanachama wa chama cha UKOMBOZI WA UMMA (CHAUMMA) hatuamini katika uchumi wa soko huria wala uchumi wa soko hodhi, tunaamini na tunapigania ujenzi wa jamii ambayo soko la kijamii ndio mwamuzi wa uchumi wa nchi kwa maslahi ya tabaka duni na hivyo utengamano wa kitaifa na usalama wa nchi yetu.

*8*

NA KWA KUWA;
Tunakumbuka kuwa waasisi wa Taifa letu walikuwa na makusudi walipopigania uhuru. Walikuwa na ndoto kuhusu jamii waliyotaka kuijenga. Walikusudia kujenga jamii ambayo pamoja na tofauti katika ziada lakini jamii inakuwa sawa katika mahitaji ya msingi na ya lazima. Kwamba tuwe na jamii ambayo watu watashindana katika ziada lakini wote ni sawa katika mahitaji ya msingi, heshima na utu.

**KWA KUWA;**
Tunaamini kuwa misingi ya soko la kijamii lenye nidhamu ndio msingi wa majibu ya changamoto zinazolikabili Taifa letu kwa sasa, tunaamini kuwa soko la kijamii ni daraja la kurejesha Taifa letu kwenye ndoto ya asili iliyokusudiwa na waasisi wa Taifa hili.

**NA KWA KUWA;**

Ni katika misingi hiyo sisi chama cha UKOMBOZI WA UMMA (CHAUMMA) tunaamini katika tamko la haki za Binadamu la mwaka 1948 linalobainisha kuhusu mahusiano ya binadamu katika jamii inayojengwa katika usawa wa mawazo na fursa sawa kwa binadamu wote kama inavyosisitizwa na kuongezewa uzito hata katika vitabu vitakatifu vya Mwenyezi Mungu.

**NA KWA KUWA ;**

Tangu nchi yetu imepata uhuru vijana wa nchi hii wameendelea kunyanyaswa na vyombo vya dola, hususani polisi ; wakiitwa **« wazururaji »** kutokana na baadhi ya sheria mbaya zilizotungwa na mkoloni na kurithiwa na Bunge letu. Sisi Chama cha Ukombozi wa Umma(CHAUMMA) tunaahidi kuliangalia hili kwa jicho na kuliondoa kabisa kwa ajili ya ustawi wa Taifa letu.

**NA KWA KUWA ;**

Nchi hii imejaliwa utajili mwingi wa asili na Mwenyezi Mungu, lakini wananchi wanaendelea kuwa fukara na uchumi wetu ukiendelea kudidimia huku wakikosa mahitaji muhimu kwenye sekta za uchumi, utamaduni, siasa na jamii ; Chama cha Ukombozi wa Umma(CHAUMMA) kimeanzishwa ili kuwaondoa wananchi kwenye lindi la umasikini na kuwaletea maisha yaliyo bora na endelevu.

**NA KWA KUWA ;**

Malengo makuu ya Chama cha UKOMBOZI WA UMMA (CHAUMMA) ni :-

♦ Kuwalinda raia na kujenga taifa lenye umoja kwa maslahi ya wote

♦ Kuhakikisha haki na usawa na kwamba kila raia ni sawa mbele ya sheria

♦ Kujenga taifa lenye ustawi unaolingana na utajiri tuliopewa na Mwenyezi Mungu

♦ Kujenga jamii inayo endeshwa kwa misingi ya demokrasia, utawala bora,uwazi,uwajibikaji na kuheshimu haki za binadamu ili kuleta ustawi kwa kila mwananchi

♦ Kuhakikisha ukombozi wa binadamu unafikiwa kama Mwenyezi Mungu Alivyokusudia Hivyo basi, sisi chama cha UKOMBOZI WA UMMA

(CHAUMMA) tumeanzisha chama hiki kufunga agano na raia wa nchi yetu Tanzania kuwa makusudi yetu ni kujenga jamii ambayo itatofautiana katika ziada lakini yenye usawa katika mahitaji ya msingi.
Ee, Mwenyezi Mungu tunakuomba.

## SURA YA KWANZA 1

**JINA, MAKAO MAKUU, KATIBA, BENDERA, NEMBO, ITIKADI, MALENGO, LUGHA RASMI.NA MISINGI YA KISIASA**

**1.1. JINA LA CHAMA** litakuwa CHAMA CHA UKOMBOZI WA UMMA (CHAUMMA)

**1.2 .MAKAO MAKUU YA CHAMA** yatakuwa Dar es Salaam na ofisi ndogo ya makao Makuu itakuwa Zanziba.

*10*

**1.3. KATIBA** ya chama ndiyo itakuwa sheria mama na mwongozo muhimu wa jinsi ya kuendesha chama na masuala mbalimbali yanayo husu chama na asasi Zake zote

**1.4. BENDERA YA CHAMA** itakuwa na rangi kuu Nne , ambazo ni :- Nyekundu, Nyeusi, Nyeupe na Njano

**1.5. NEMBO YA CHAMA** itakuwa na alama moja ambayo ni kiganja cha mkono kilicho kunjwa ikimaanisha umoja na mshikamano wa Taifa.

**1.6. ITIKADI YETU NI DEMOKRASIA YA KIJAMII**, ambayo misingi yake ni :- Uhuru, umoja, ukweli, haki, amani, usawa mbele ya sheria, ustawi wa jamii na maendeleo kwa wote.

**1.7. LUGHA RASMI** ya chama itakuwa Kiswahili na lugha nyingine zitatumika itakapokuwa hapana budi kufanya hivyo.

**1.8. Falsafa ya Chama ni:** Umoja wa kitaifa, ukweli, uwazi, mshikamano na ujenzi wa jamii ya kidemokrasia iliyo huru na haki inayotendeka kwa wakati.

## SURA YA PILI

## 2.0. MALENGO NA MADHUMUNI YA MISINGI YA KISIASA YA CHAMA

### MALENGO YA CHAMA

**2.1. Malengo ya Chama ni kama ifuatavyo:**

**2.1.1.** Kuwalinda raia na Kujenga taifa lenye umoja kwa maslahi ya wote

**2.1.2.** Kuhakikisha haki na usawa na kwamba kila raia ni sawa mbele ya sheria

2.1.3. Kujenga taifa lenye ustawi unaolingana na utajiri tuliopewa na Mwenyezi Mungu .

*2.1.4.* Kujenga jamii inayo endeshwa kwa misingi ya demokrasia, utawala bora,uwazi,uwajibikaji na kuheshimu haki za binadamu ili kuleta ustawi kwa kila mwananchi

2.1.5. Kuhakikisha ukombozi wa binadamu unafikiwa kama Mwenyezi Mungu Alivyokusudia

*11*

### 2.2 MADHUMUNI YA CHAMA

**Madhumuni ya Chama yatakuwa Kama ifuatavyo:-**

**2.2.1**. Kupokea hatamu za uongozi wa dola kutoka kwa wananchi kwa njia ya uchaguzi huru na haki.

**2.2.2.** Kujenga demokrasia ya kweli ya kijamii yenye kufuata misingi ya utawala bora na kuheshimu haki za binadamu.

**2.2.3.** Kuhakikisha na kutetea dhana ya kuwa umma ndiyo chimbuko la mamlaka ya dola na maendeleo ya kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kijamii.

**2.2.4**. Kuzingatia mahitaji maalumu ya watoto, wanawake, wazee na walemavu katika ya maendeleo na kuwalinda dhidi ya uwovu wanaoweza kutendewa,ili waweze kujiendeleza na kushiriki katika shughuli mbalimbali sawa na watu wengine.

**2.2.5.** Kuheshimu kazi na shughuli halali za watu binafsi katika nyanja zote za jamii na uchumi.

2.2.6. Kuunga mkono juhudi za vyama mbalimbali duniani katika kutetea ustawi wa jamii na vyenye itikadi inayo fanana na chama chetu .

2.2.7.Kuwa na uongozi unaoheshimu watu wake ,katiba ya nchi,na utawala wa sheria na haki za binadamu kwa mujibu wa tangazo la Umoja wa mataifa la mwaka 1948 kuhusu Haki za binadamu na katiba ya nchi yetu.

**2.2.8.** Kuhakikisha kuwa serikali inasimamia kikamilifu na kuweka mazingira bora na endelevu kwa kila mwananchi kufanya kazi kwa bidii ili kujiletea maendeleo.

2.2.9. Kutoa kipaumbele au upendeleo wa makusudi kwa wananchi ambao wako nyuma kimaendeleo kwa sababu zilizo nje ya uwezo wao ili kuinua maisha yao.

**2.2.10.** Kuwa na tasnia huru ya habari.

2.2.11.Kuwapo mazingira safi na salama, kulinda na kutunza mazingira kwa maslahi ya sasa na vizazi vijavyo kwa ajili ya uhai wa binadamu na viumbe vingine.



2.2.12. Kuwa na jamii isiyo na ubaguzi wa rangi, kabila, dini au jinsia.

2.2.13. Kuweka kipaumbele katika uhusiano wa kimataifa pale ambapo kuna maslahi makubwa kwa taifa letu.

**2.2.14**. Kuwa na Mahakama huru zenye mamlaka ya kutoa haki kwa wananchi na kuzingatia haki za binadamu

**2.2.15**. Kufanya lugha ya Kiswahili kuwa miongoni mwa lugha kubwa duniani.

# SURA YA TATU

## 3.0 UANACHAMA

### 3.1. Kujiunga na Chama:

**Kujiunga na chama mtu anatakiwa kutimiza masharti yafuatayo:-**

**3.1.1.** Awe ni raia wa Tanzania

**3.1.1.1.** Awe anaye amini uwepo wa Mungu

***3.1.1.2.*** Awe na umri unaomruhusu kupiga kura kwa mjibu wa katiba ya nchi

**3.1.1.3.** Awe na akili timamu

**3.1.1.4**. Awe anaamini, anakubali itikadi, malengo, madhumuni, katiba, kanuni,taratibu na miongozo ya chama

**3.1.1.5**. Asiwe mwanachama wa chama kingine cha siasa

**3.1.1.6.** Akikubaliwa anunue kadi ya chama na kulipa ada zote za Chama zinazostahili. Katibu wa ngazi inayohusika amworodheshe kwenye daftari la wanachama.

**3.1.2. Haki za Mwanachama.**

**3.1.2.1.** Kuchagua na kuchaguliwa katika nafasi ya uongozi wa Chama wa ngazi yoyote .

3.1.2.2. Kupata habari zote zilizojadiliwa na kutolewa uamuzi na wanachama katika kumbukumbu za vikao vinavyo muhusu.

**3.1.2.3**. Kutoa hoja za mapendekezo ya kusahihisha na kuweka sawa maongozi ya Chama bila hofu wala upendeleo. Iwe ni kwa nia njema na kwa maslahi ya kukijenga chama Hoja zitatolewa kwa kuwasilishwa kwa maandishi kwa Katibu wa Chama wa ngazi husika moja kwa moja bila hofu yoyote.



**3.1.2.4.** Kuwa na haki ya kujitetea mbele ya kikao cha Chama kinachohusika katika malalamiko au madai yoyote; na kuwa na haki ya kukata rufaa kwenye vikao vya juu iwapo mhusika hakuridhika na uwamuzi wa vikao vya chini..

**3.1.3 Wajibu wa Mwanachama:**

3.1.3.1. Kulipa ada za kila mwezi, mwaka au miaka ili kufanikisha shughuli za Chama.

3.1.3.2. Kuwa tayari kufanya shughuli za chama bila kutegemea malipo na kuwa tayari kujitoa kwa hali na mali ili kukijenga na kukiimarisha Chama.

3.1.3.3. Kushiriki kikamilifu katika shughuli na uongozi wa Chama na kueneza sera na programu za Chama wakati wote na awe tayari kukitetea chama na

sera zake popote

3.1.3.4. Kuwa na uhuru wa maoni na kuheshimu tofauti za maoni pamoja na kuheshimu

uamuzi wa pamoja.

3.1.3.5. Kuwa mwaminifu na mwadilifu kwa matendo na kwa kusema na kutenda mambo ya kujenga na kuimarisha chama.

3.1.3.6. Kuwa mstari wa mbele katika kutetea haki za binadamu na kupinga uwonevu, udhalimu , rushwa na ubaguzi wa kila aina na matendo yanayo haribu maadili ya jamii.

3.1.3.7. Kujifunza masuala ya jamii kuelewa matatizo ya watu na kiini cha matatizo hayo na kujitahidi kutafuta majibu ya matatizo hayo kwa kushirikiana na wanaohusika.

3.1.3.8. Kukilinda chama dhidi ya mitafaruku, majungu, vitendo vya kukigawa na kukidhoofisha



**3.1.4 Kuondoka katika Chama :**

Uanachama wa mtu utakoma pale mambo yafuatayo yakitokea:-

3.1.4.1. Kujiuzulu kwa hiari yake mwenyewe.

3.1.4.2. Kwa kujiunga na chama kingine cha Siasa.

3.1.4.3. Kwa kufariki dunia

3.1.4.4.kufukuzwa uanachama

3.1.4.5. Aliyeondoka katika chama anaweza kuwa mwanachama tena kwa kuomba upya Uanachama kupitia tawi husika.

3.1.4.6. Aliyefariki dunia, Msimamizi wa mirathi /au ndugu za marehemu husikaWatawajibika kurejesha mali àu amana za Chama alizokuwa nazo mwanachama mpaka siku kifo Kilipomfika.

3.1.4.7. Aliyejiuzulu endapo atakubaliwa kurejea katika Chama atawajibika kununua kadimpya na kulipa michango yote ya nyuma.

3.1.4.8. Anayeondoka katika chama hatarejeshewa ada au mchango wowote

alioutoa.

3.1.4.9. Mwanachama kupeleka chama Mahakamani. .

**SURA YA NNE 4**

**4.0. UONGOZI KATIKA CHAMA**

**4.1.1. Sifa za kiongozi:**

**4.1.1.1.** Awe ana umri unaoruhusiwa kisheria kuwa kiongozi katika nafasi husika.

4.1.1.2. Awe mchapakazi na mwenye uwezo wa kuongoza.

4.1.1.3. Awe mtu mwenye uadilifu usio kuwa na mashaka.

4.1.1.4. Awe na moyo na uwezo wa kufanya kazi na makundi mbali mbali ya jamii katika mazingira ya aina mbali mbali.

4.1.1.5. Awe mtu aliye mstari wa mbele katika kujua matatizo ya jamii na kuyatafutia ufumbuzi.

*15*

4.1.1.6. Awe ni mzalendo na shujaa katika kutetea maslahi ya Taifa.

4.1.1.7. Awe mtu mwenye msimamo thabiti katika kukisimamia Chama.

4.1.1.8. Awe mwajibikaji na mwenye kuheshimu vikao.

**4.1.2 Kuacha Uongozi:**

Kiongozi ataacha uongozi ikiwa mambo yofuatayo yatatokea:-

**4.1.2.1.** Muda wa uongozi kumalizika.

**4.1.2.2.** Kujiuzulu mwenyewe kwa sababu zake binafsi.

**4.1.2.3.** Kujiuzulu iwapo wale anaowaongoza wameishiwa imani na uongozi wake kwa kupigiwa kura na robo tatu ya wajumbe halal iwa kikao husika.

**4.1.2.4**. Kusimamishwa au kuondolewa iwapo kiongozi amekiuka katiba, kanuni taratibu, maadili, na sera za Chama.

**4.1.2.5.** Akitiwa hatiani na kufungwa kifungo cha mwaka mmoja.

**4.1.2.6.** Kupatwa na maradhi yanayoondoa uwezo wake wa kufanya kazi

**4.1.2.7.** Kupoteza sifa ya uanachama

# SURA YA TANO 5

## 5.0 NGAZI NA VIKAO VYA CHAMA

### 5.1. Muundo wa ngazi na Vikao vya Chama:

Vikao vya chama vitakuwa Kama ifuatavyo:-

**5.1.1.** Chemchemi ambayo ni ngazi ya kwanza yan chini ya chama inayoundwa na wanachama walioko kwenye ngazi hiyo ya kwanza.

**5.1.2.** Tawi ambayo ni ngazi ya pili baada ya chemchemi ambayo inayoundwa na wanachama alioko kwenye tawi hilo

**5.1.3**. Kata/Wadi ambayo ni ngazi ya tatu ya chini baada ya tawi ambayo inayoundwa na wanachama walioko kwenye kata hiyo

*16*

**5.1.4**. Jimbo ambayo ni ngazi ya nne ya chini baada ya kata ambayo inayoundwa na wanachama walioko kwenye kata za jimbo la uchaguzi.

**5.1.5**. Mkoa ambayo ni ngazi ya tano ya chini baada ya jimbo ambayo inayoundwa na wanachama walioko kwenye majimbo husika ya mkoa huo.

**5.1.6.** T**aifa** ambayo ni ngazi ya juu ya chama ambayo inayoundwa na wanachama walioko kwenye mikoa yote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

### 5.2. Ngazi ya Chemchemi.

Kutakuwa na Chemchemi kama ngazi ya kwanza katika muundo wa chama.

**5.2.1**. Kutakuwa na wanachama wasiopungua watano

**5.2.**2. Kutakuwa na kikao kimoja ambacho ni Mkutano wa Chemchemi isipokuwa penye wanachama zaidi ya watano yaani 10 nakuendelea kutakuwa na kikao cha utendaji.

5.2.3.kutakuwa na wajumbe wa Mkutano wa Chemchemi

5.2.4. Itakuwa na mwenyekiti wa Chemchemi.

5.2.4. Itakuwa na Katibu wa Chemchemi.

5.2.4. kutakuwa na wanachama wote wa Chemchemi

**5.3. Kazi za Mkutano wa Kamati ya Utendaji wa Chemchemi:**

**5.3.1**. Kumchagua Mwenyekiti

**5.3.2**. Kusimamia shughuli za Chama

**5.3.3**. Kujadili na kupitisha bajeti

**5.3.4**. Kutekeleza maamuzi na maelekezo ya kikao cha juu yake

**5.3.5**.Mkutano utafanyika walau mara moja kila mwezi .

5**.4. Kazi za Mwenyekiti wa Chemchemi**

5.4.1. Kuwa msimamizi mkuu wa shughuli za kila siku

5.4.2. Kuwa msemaji na mhamasishaji mkuu wa chama

5.4.3. Kuongoza mikutano na vikao

**5.5. Kazi za Katibu wa Chemchemi**

5.5.1. Kuwa mtendaji mkuu



5.5.2. Kutunza daftari la orodha na kumbukumbu za wanachama

5.5.3. Kukusanya ada na mapato mengine ya chama na kuyawasilisha kwa Mweka hazina wa Tawi

5.5.4. Kuwa mdhibiti mkuu wa mali za chama

5.5.5. Kuwajibika na kutoa taarifa kila mwezi kuhusu utendaji wa shughuli za Chama kwa wanachama na kwenye Tawi.

**5.6. Ngazi ya Tawi**

Kutakuwa na Tawi katika kila eneo la serikali ya mtaa kwa mijini na Tawi katika kila eneo la serikali ya Kijiji

5.6.1.**Vikao vya Tawi:**

5.6.1.1.Mkutano mkuu wa Tawi.

5.6.1.2.Kamati ya Utendaji ya Tawi.

5.6.1.3. Sekretariati ya Tawi.

5.6.2. **Wajumbe wa Mkutano Tawi**

5. .6.2.1.Mwenyekiti wa Tawi

5.6.2.2. Mweka hazina.

5.6.2.3. Afisa habari na taarifa kwa umma wa Tawi

5.6.2.4. Viongozi wote wa serikali ya Mtaa/Kijiji waliochaguliwa kwa tiketi ya Chama

5.6.2.5. Wenyeviti wa Chemchemi.

5.6.2 .6. Wenyeviti na Makatibu wa Mabaraza ya Chama.

5.6.2.7. Wanachama wote waliopo katika Tawi

**5.6.3. Kazi za Mkutano Mkuu wa Tawi.**

**5.6.3**.1. Kumchagua Mwenyekiti wa Tawi unapofika wakati wa uchaguzi.

5.6.3.2.kumchagua katibu wa kamati Tendaji ya Tawi Miongoni mwa wajumbe waliochaguiwa.

**5.6.3**.3. Kumchagua Mweka Hazina na Afisa habari na taarifa kwa Umma



**5.6.3**.4. Kupokea na kujadili taarifa ya Kamati ya Utendaji ya Tawi na ya Mabaraza ya Chama na kutoa maamuzi au mwongozo ama maelekezo kwa utekelezaji.

**5.6.3**.5. Kuwapatia mwongozo na maelekezo wawakilishi wa Chama walio katika serikali za mitaa/kijiji

**5.6.3**.6. Kusilikilza na kutoa mapendekezo kwa ngazi ya juu kuhusu masuala ya nidhamu kwa wanachama

**5.6.3**.7. Kutoa mapendekezo ngazi ya juu kuhusu masuala ya kijamii,kiuchumi na kisiasa yanayohitaji hatua za Chama ngazi ya juu.

**5.6.3**.8. Kuchagua wajumbe sita watakaokuwa wajumbe wa kamati ya utendaji ya Tawi miongoni mwao watatu wawe wanawake.

**5.6.3**.9. Kuchagua wajumbe wawili watakao kuwa wajumbe wa Mkutano mkuu wa Kata.

**5.6.3**.10. Kuchagua wajumbe 2 wa Kamati ya Utendaji ya Tawi

**5.6.3**.11. Kupima utekelezaji wa shughuli za Chama katika Tawi hilo

**5.6.3**.12. Mkutano mkuu wa Tawi utafanyika angalau mara moja kila baada ya miezi mitatu..

### 5.6.4. Kamati ya Utendaji ya Tawi

Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Tawi

5.6.4.1. Mwenyekiti

5.6.4.2. Katibu wa Tawi

5.6.4.3. Afisa habari na taarifa kwa umma

5.6.4.4. Wenyeviti wote wa mabaraza ya chama katika tawi hilo

5.6.4.5. Wajumbe wawili waliochaguliwa na Mkutano mkuu wa Tawi, ambapo mmoja ni mwanamke

5.6.4.6 Wenyeviti wote wa vijiji/mtaa waliochaguliwa kwa tiketi ya CHAUMMA

5.6.4.7 Wenyeviti na makatibu wa chama wa chemchemi

*19*

### 5.6.5. Kazi za Kamati ya Utendaji ya Tawi

**5.6.5**.1. Kusimamia shughuli za kila siku za Chama.

**5.6.5**.2. Kumchagua Katibu wa Tawi baada ya kujaza fomu ya kugombea nafasi hiyo na pia inauwezo wa kumuondoa madarakani katibu wa Tawi.

**5.6.5**.3. Kuwahimiza wananchi kujiandikisha na kufanya kampeni wakati wa uchaguzi ili kuhakikisha kuwa chama kinapata ushindi.

**5.6.5**.4 Kutafuta wanachama wapya na kuongeza wigo wa kuungwa mkono

**5.6.5**.5. Kuhakikisha ustawi wa Chemchemi zilizopo katika Tawi hilo.

**5.6.5**.6. Kuwaelekeza wananchi jinsi ya kupata, kutetea na kulinda haki zao na kupinga uonevu unaoweza kufanywa na serikali au kikundi chochote.

**5.6.5**.7. Kujadili maombi ya wanaoomba kugombea uongozi wa serikali za mitaa /katika Chama na kuyawasilisha kwa Katibu wa Kata/Wadi.

**5.6.5**.8. Kuongoza katika eneo lake, harakati za kupinga uonevu unaoweza kufanywa na

serikali au kikundi chochote.

**5.6.5**.9. Kushughulika na nidhamu ya viongozi na wanachama wa Tawi hilo na kuchukua hatua za kinidhamu kwa wanachama.

**5.6.5**.10. Kumjadili aliyeondoka katika chama na ambaye ameomba kurudi katika Chama na kutoa mapendezo kwa Kamati ya Kata/Wadi

**5.6.5**.11. Kujadili maombi ya wanaoomba kugombea uongozi wa serikali za mitaa

**5.6.5**.12. Kujadili na kupitisha bajeti ya Chama ya Tawi.

**5.6.5**.13. Kupokea, kujadili na kupitisha taarifa ya kila mwaka ya maendeleo ya kila baraza la Chama.

**5.6.5**.14. Kukieneza Chama katika Tawi.

5.13.15. Kutekeleza sera na kazi za Chama katika Tawi hilo

**5.6.5**.16 Kuwaandaa wanachama kushirikiana na wananchi wengine katika kuleta demokrasia ya kweli na maendeleo kwa kushirikiana na vyama vya kijamii.

5.6.5.17 Kumchagua katibu wa tawi na kumuondoa pale atakapoenda kinyume na katiba,kanuni na maadili ya chama.



5.6.5.18 Kumchagua Mweka hazina na Afisa habari na taarifa kwa Umma.

**5.6.6. Wajumbe wa Sekretariati**

**5.6.6.**1. Katibu wa Tawi ndiye mwenyekiti wa Sekretariati

**5.6.6.**2. Afisa habari na taarifa kwa umma

**5.6.6.**3. Mweka hazina wa Tawi

**5.6.6.**4. Makatibu watatu wa mabaraza ya wazee, wanawake na vijana wa Tawi na pia Watamchagua katibu wa sekretariati miongoni mwao.

## 5.6.7. Kazi za Sekretariati

**5.6.7**.1. Kuandaa dondoo (agenda) na nyaraka za kikao cha Kamati ya Utendaji na mkutano mkuu

**5.6.7**.2. Kuandaa bajeti

**5.6.7**.3. Utekelezaji wa maamuzi na maelekezo ya kamati ya utendaji

**5.6.7**.4. Utekelezaji wa kazi za kila siku za uendeshaji wa shughuli za Chama.

**5.6.8.Kazi za Mwenyekiti wa Tawi.**

**5.6.8**.1. Kuwa msimamizi mkuu wa shughuli za kila siku za Chama katika Tawi.

**5.6.8**.2. Kuwa msemaji na mhamasishaji mkuu wa Chama katika Tawi.

**5.6.8**.3. Kuongoza vikao vya Chama vya Tawi.

**5.6.9. Kazi za Katibu wa Tawi.**

**5.6.9**.1. Kuwa mtendaji mkuu wa Chama katika Tawi.

**5.6.9**.2. Kutunza daftani la orodha na kumbukumbu za Chemchemi na wanachama waliopo katika Tawi hilo.

**5.6.9**.3. Kutunza kumbukumbu za mali za Chama zisizo ondosheka na zinazo ondosheka na kumbukumbu nyinginezo muhimu.

**5.6.9**.4. Kusimamia vyanzo vya mapato na miradi ya Chama iliyopo katika Tawi hilo.

**5.6.9**.5 . Kuwa mdhibiti mkuu wa mali za Chama za Tawi.

**5.6.9.6**. Kuwajibika na kutoa taarifa za kila mwezi kuhusu utendaji wa kazi za Chama katika Tawi kwa ngazi ya Kata/ Wadi.



**5.6.10. Kazi za Mweka Hazina wa Tawi:**

5.6.10.1. Kubuni/kutafuta fedha kwa ajili ya Chama.

5.6.10.2. Kuweka kumbukumbu za mapato na matumizi ya Chama.

5.6.10.3. Kuandaa bajeti ya Chama ya Tawi na kuwasilisha kwenye kamati ya utendaji ya Tawi.

5.6.10.4. Kutoa taarifa ya mapato na matumizi ya Chama.

**5.6.11. Kazi za Afisa habari na taarifa kwa umma.**

**5.6.11**.1. Kukitangaza Chama ndani na nje ya Tawi

**5.6.11**.2. Kukieneza Chama ndani na nje ya Tawi

**5.6.11**.3. Ndiye mtoa habari zinazohusu chama kwa umma katika Tawi

**5.7. Ngazi ya kata/Wadi**

Kutakuwa na **Kata/Wadi** katika kila eneo la serikali ya mtaa kwenye Kata kwa

upande wa Bara na Wadi kwa upande wa Zanzibar.

**5.7.1.Vikao vya Kata:**

**5.7.1**.1. Mkutano mkuu wa Kata:

**5.7.1**.2. Kamati ya Utendaji ya Kata:

**5.7.1**.3. Kamati ya Sekretariati ya Kata

**5.7.2. Wajumbe wa Mkutano Mkuu Kata:**

**5.7.2**.1.Mwenyekiti wa Kata

**5.7.2**.2. Katibu wa Kata

**5.7.2.** 3.Afisa habari na taarifa kwa umma wa Kata

**5.7.2**.4. Mweka hazina.

**5.7.2.**5.Viongozi wote wa serikali ya Mtaa/Kijiji waliochaguliwa kwa Tiketi ya chama

**5.7.2**.6.Wenyeviti wa Chemchemi.

**5.7.2.** 7.Wenyeviti na Makatibu wa Mabaraza ya Chama.



**5.7.2.**8.Wajumbe 2 kutoka kila tawi katika Kata hiyo

**5.7.3. Kazi za Mkutano Mkuu wa Kata.**

**5.7.3.**1. Kumchagua Mwenyekiti unapofika wakati wa uchaguzi.

**5.7.3.**.3 . Kumchagua Mweka Hazina na Afisa habari na taarifa kwa Umma

**5.7.3.**.4. Kuchagua wajumbe wawili watakao kuwa wajumbe wa Mkutano mkuu wa Jimbo.

**5.7.3.**.5. Kuchagua wajumbe 2 wa Kamati ya Utendaji ya Kata

**5.7.3.**.6. Kupokea na kujadili taarifa ya Kamati ya Utendaji ya Kata na ya Mabaraza ya Chama na kutoa maamuzi au mwongozo ama maelekezo kwa utekelezaji.

**5.7.3.**.7. Kuwapatia mwongozo na maelekezo wawakilishi wa Chama walio katika serikali za mitaa

**5.7.3.**8. Kusilikilza na kutoa mapendekezo kwa ngazi ya juu kuhusu masuala ya nidhamu Nidhamu kwa wanachama

**5.7.3**.9. Kutoa mapendekezo ngazi ya juu kuhusu masuala ya kijamii,kiuchumi na kisiasa

**5.7.3**.10. Kupima utekelezaji wa shughuli za Chama katika Kata hiyo

**5.7.3.**.11. Mkutano mkuu wa Kata utafanyika angalau mara moja kila baada ya miezi mitano.

### 5.7.4. Kamati ya Utendaji ya Kata

Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Kata ni kama ifuatavyo:-

**5.7.4..1.** Mwenyekiti wa Kata

**5.7.4..2.** Katibu wa Kata

**5.7.4..3**. Afisa habari na taarifa kwa umma wa Kata

**5.7.4..4.** Wenyeviti wote wa mabaraza ya chama katika Kata hilo

**5.7.4..5.** Wajumbe wawili waliochaguliwa na Mkutano mkuu wa Kata, ambapoAmbapo mmoja ni mwanamke

5.7.4.6. Wenyeviti na Makatibu wa chama ngazi ya tawi

### 5.7.5. Kazi za Kamati ya Utendaji ya Kata:-



**5.7.5.1.** Kusimamia shughuli za kila siku za Chama.

**5.7.5.2.** Kuwahimiza wananchi kujiandikisha na kufanya kampeni wakati wa uchaguzi ili kuhakikisha kuwa chama kinapata ushindi.

**5.7.5.3** Kutafuta wanachama wapya na kuongeza wigo wa kuungwa mkono

**5.7.5.4** Kuhakikisha ustawi wa matawi yaliyo katika Kata.

**5.7.5.5.** Kuwaelekeza wananchi jinsi ya kupata, kutetea na kulinda haki zao na kupinga uonevu unaoweza kufanywa na serikali au kikundi chochote.

**5.7.5.6.** Kumjadili aliyeondoka katika chama na ambaye ameomba kurudi katika Chama na Kutoa mapendezo kwa Kamati ya Utendaji ya Jimbo.

**5.7.5.7.**. Kushughulika na nidhamu ya wanachama wa Kata hiyo na kuchukua hatua za nidhamu kwa wanachama.

**5.7.5.8** Kukieneza Chama katika Kata.

**5.7.5.9.** Kupokea, kujadili taarifa ya kila mwaka maendeleo ya Kamati ya Utendaji ya Tawi

na ya kila baraza la Chama na kutoa maamuzi au mwongozo ama maelekezo kwa utekelezaji.

. **5.7.5.10** Kusimamia matumizi ya fedha

**5.7.5..11.** Kumjadili aliyeondoka katika chama na ambaye ameomba kurudi katika Chama Nakutoa mapendekezo kwa kamati ya Kata/Wadi

**5.7.5..12.** Kujadili maombi ya wanaoomba kugombea uongozi wa serikali za mitaa /katika Chama .

**5.7.5. 13**. Kujadili na kupitisha bajeti ya Chama ya Kata.

**5.7.5..14.** Kusimamia matumizi ya fedha

**5.7.5. 15.** Kuwa na mpango mkakati kwa ajili ya kukiimarisha Chama katika Kata.

**5.7.5.16** Kutekeleza sera na kazi za Chama katika Kata hiyo

**5.7.5.17** Kuwaandaa wanachama kushirikiana na wananchi wengine katika kuleta demokrasia ya kweli na maendeleo kwa kushirikiana na vyama vya kijamii.

5.7.5.18 Kumchagua katibu wa chama ngazi ya kata

5.7.5.19 Kuwachagua Mweka hazina na Afisa habari kwa umma ngazi ya kata



**5.7.6. Wajumbe wa Sekretariati ya Kata:**

Wajumbe wa Sekretariati ya Kata watakuwa kama ifuatavyo:-

**5.7.6.1**. Katibu wa Kata ndiye mwenyekiti wa Sekretariati

**5.7.6.2.** Afisa habari na taarifa kwa umma

**5.7.6.3.** Mweka hazina wa Kata

**5.7.6.4** Makatibu watatu wa mabaraza ya wazee, wanawake na vijana wa Kata na pia watamchagua katibu wa sekretariati miongoni mwao.

## 5.7.7. Kazi za Sekretariati ya Kata.

5**.7.7**.1. Kuandaa dondoo (agenda) na nyaraka za kikao cha Kamati ya Utendaji na mkutano Mkuu

**5.7.7**.2. Kuandaa bajeti ya Kata.

**5.7.7**.3. Utekelezaji wa maamuzi na maelekezo ya kamati ya utendaji

**5.7.7**.4. Utekelezaji wa kazi za kila siku za uendeshaji wa shughuli za Chama.

**5.7.8.Kazi za Mwenyekiti wa Kata.**

**5.7.8.1.** Kuwa msimamizi mkuu wa shughuli za kila siku za Chama katika Kata.

**5.7.8.2.** Kuwa msemaji na mhamasishaji mkuu wa Chama katika Kata.

**5.7.8.3.** Kuongoza vikao vya Chama vya Kata.

**5.7.9. Kazi za Katibu wa Kata/Wadi.**

**5.7.9.1**. Kuwa mtendaji mkuu wa Chama katika Kata.

**5.7.9.2.** Kutunza daftani la orodha na kumbukumbu za wanachama waliopo katika Kata hiyo.

**5.7.9.3.**Kutunza kumbukumbu za mali za Chama zisizo ondosheka na zinazo ondosheka na kumbukumbu nyinginezo muhimu.

**5.7.9.4.** Kusimamia vyanzo vya mapato na miradi ya Chama iliyopo katika Kata hiyo.

**5.7.9.5.** Kuwa mdhibiti mkuu wa mali za Chama za Kata hiyo.

**5.7.9.6.** Kuwajibika na kutoa taarifa za kila mwezi kuhusu utendaji wa kazi za Chama katika Kata hiyo kwa ngazi ya Kata/ Wadi.



**5.7.10.Kazi za Mweka Hazina wa Kata**

**5.7.10.1.** Kubuni/kutafuta fedha kwa ajili ya Chama.

**5.7.10.2.** Kuweka kumbukumbu za mapato na matumizi ya Chama.

**5.7.10.3.** Kuandaa bajeti ya Chama ya Kata na kuwasilisha kwenye kamati ya utendaji ya

**5.7.10.4.** Kutoa taarifa ya mapato na matumizi ya Chama.

**5.7.11. Kazi za Afisa habari na taarifa kwa umma wa Kata.**

**5.7.11.1**. Kukitangaza Chama ndani na nje ya Kata hiyo.

**5.7.11.2**. Kukieneza Chama ndani na nje ya Kata hiyo.

**5.7.11.3.** Ndiye mtoa habari zinazohusu chama kwa umma katika Kata hiyo.

**5.8. Ngazi ya Jimbo**

**5.8.1 Jimbo litakuwa na vikao vifuatavyo:**

**5.8.1.1.**Mkutano mkuu wa Jimbo

**5.8.1.2.** Kamati ya Utendaji ya Jimbo

**5.8.1.3**.Kamati ya Sekretariati ya Jimbo

**5.8.2.Wajumbe wa Mkutano Mkuu Jimbo:**

**5.8.2.1**.Mwenyekiti wa Jimbo

**5.8.2.2**.Katibu wa Jimbo

**5.8.2.3.**Afisa habari na taarifa kwa umma wa Jimbo

**5.8.2.4.**Mweka hazina wa Jimbo.

**5.8.2.5.**Mbunge/Mwakilishi wa Jimbo/Mbunge viti maalumu kupitia CHAUMMA

**5.8.2.6.** Madiwani waliochaguliwa kwa tiketi ya CHAUMMA.

**5.8.2.7**.Wenyeviti na Makatibu wa Mabaraza katika Jimbo

**5.8.2.8.**Wenyeviti na Makatibu wa Chama wa Tawi na Kata katika Jimbo.

**5.8.2.9.**Wenyeviti na makatibu wa mabaraza wa Kata katika Jimbo

**5.8.2.10.**Wajumbe 2 kutoka kila kata katika Jimbo hilo

*26*

**5.8.3. Kazi za Mkutano Mkuu wa Jimbo.**

5.8.3.1 Kuchagua Mwenyekiti wa Jimbo unapofika wakati wa uchaguzi.

5.8.3.3 Kuchagua Mweka Hazina na Afisa hababari na taarifa kwa Umma

**5.8.3.5 .**Kuchagua wajumbe nne watakaokuwa wajumbe wa Halmashauri ya Jimbo miongoni mwao wawili wawe wanawake

**5.8.3.6.**Kuchagua wajumbe wawili watakao kuwa wajumbe wa Mkutano mkuu wa Mkoa.

**5.8.3.7.**Kuchagua wajumbe 2 wa Kamati ya Utendaji ya Jimbo

**5.8.3**.8..Kutoa mapendekezo ngazi ya juu kuhusu masuala ya kijamii,kiuchumi na kisiasa yanayohitaji hatua za Chama ngazi ya juu.

**5.8.3.9.** Kusilikiliza na kutoa mapendekezo kwa ngazi ya juu kuhusu masuala ya nidhamu

kwa mwanachama

**5.8.3.10**.Kumchagua mjumbe 1 atakayekuwa mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa

**5.8.3.11**.Kupima utekelezaji wa shughuli za Chama katika Jimbo hilo

**5.8.3.12**.Kutoa maelekezo yanayofaa kwa ajili ya maendeleo ya chama katika Jimbo hilo.

**5.8.3.13.** Kuwapatia mwongozo na maelekezo wawakilishi wa Chama walio katika serikali za mitaa

**5.8.3.14.** Mkutano wa Jimbo utafanyika walau mara moja kwa mwaka.

5.8.3.15.kumchagua katibu wa Jimbo Miongoni mwa wajumbe waliochaguiwa.

### 5.8.4. Kamati ya Utendaji ya Jimbo

5.8.4.1. Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Jimbo watakuwa kama ifuatavyo

5.8.4.1.**1**.Mwenyekiti wa Jimbo

5.8.4.1.**2.**Katibu wa Jimbo

5.8.4.1.**.3.**Afisa habari na taarifa kwa umma wa Jimbo

5.8.4.1.**4**.Wenyeviti wote wa mabaraza ya chama wa Kata katika Jimbo hilo

5.8.4.1.**5.**Wajumbe wawili kutoka kila Kata waliochaguliwa na Mkutano mkuu

wa kata ambapo mmoja ni mwanamke

5.8.4.1.6. Wenyeviti na makatibu wa chama ngazi ya kata

5.8.4.1.7 Wenyeviti na makatibu wa madiwani waliochaguliwa kupitia chama na wanaishi Jimboni.

5.8.4.1.8 Mbunge / Mwakilishi anaeishi jimbo husika

### 5.8.5. Kazi za Kamati ya Utendaji ya Jimbo:-

5.8.5.1 Kusimamia shughuli za kila siku za Chama.

5.8.5.2 Kuwahimiza wananchi kujiandikisha na kufanya kampeni wakati wa

uchaguzi ili kuhakikisha chama kinapata ushindi.

5.8.5.3 Kutafuta wanachama wapya na kuongeza wigo wa kuungwa mkono

5.8.5.4 Kuhakikisha ustawi wa matawi yaliyo katika Kata.

5.8.5.5 Kuwaelekeza wananchi jinsi ya kupata, kutetea na kulinda haki zao na kupinga uonevu unaoweza kufanywa na serikali au kikundi chochote.

5.8.5.6 Kumjadili aliyeondoka katika chama na ambaye ameomba kurudi katika Chama na kutoa mapendezo kwa Kamati ya Utendaji ya Jimbo.

5.8.5.7 Kushughulika na nidhamu ya wanachama wa Kata hiyo na kuchukua hatua za nidhamu Kwa wanachama.

5.8.5.8 Kukieneza Chama katika Kata.

5.8.5.9 Kupokea, kujadili taarifa ya kila mwaka maendeleo ya Kamati ya Utendaji ya Tawi na ya kila baraza la Chama na kutoa maamuzi au mwongozo ama maelekezo kwa utekelezaji.

5.8.5.10 Kusimamia matumizi ya fedha 28

5.8.5.11 Kumjadili aliyeondoka katika chama na ambaye ameomba kurudi katika Chama Na kutoa mapendekezo katika kamati ya jimbo

5.8.5.12 Kujadili maombi ya wanaoomba kugombea uongozi wa serikali za mitaa /katika Chama

5.8.5.13 Kujadili na kupitisha bajeti ya Chama ya Jimbo.

5.8.5.14 Kusimamia matumizi ya fedha

5.8.5.15 Kuwa na mpango mkakati kwa ajili ya kukiimarisha Chama katika Kata.

5.8.5.16 Kutekeleza sera na kazi za Chama katika Kata hiyo

5.8.5.17 Kuwachagua mweka hazina na afisa habari kwa umma ngazi ya Jimbo

**5.8.5.18**.Kuwaandaa wanachama kushirikiana na wananchi wengine katika kuleta demokrasia ya kweli na maendeleo kwa kushirikiana na vyama vya kijamii.

**5.8.6. Sekretariati ya Jimbo**

5.8.6.1. Wajumbe wa Sekretariati ya Jimbo ni kama ifuatavyo:-

5.8.6.1**.1.** Katibu wa Jimbo ndiye mwenyekiti wa Sekretariati

5.8.6.1**.2.** Afisa habari na taarifa kwa umma wa Jimbo

5.8.6.1**.3**. Mweka hazina wa Jimbo

5.8.6.1**.4.** Makatibu watatu wa mabaraza ya wazee, wanawake na vijana wa Jimbo na pia Watamchagua katibu wa sekretariati miongoni mwao.

**5.8.7. Kazi za Sekretariati ya Jimbo.**

5.8.7.1 Kuandaa dondoo (agenda) na nyaraka za kikao cha Kamati ya Utendaji na mkutano mkuu

5.8.7.2 Kuandaa bajeti

5.8.7.3 Utekelezaji wa maamuzi na maelekezo ya kamati ya utendaji

5.8.7.4 Utekelezaji wa kazi za kila siku za uendeshaji wa shughuli za Chama.



**5.8.8. Kazi za Mwenyekiti wa Jimbo**

**5.8.8.1.** Mwenyekiti wa jimbo ndiye msimamizi mkuu wa shughuli za kila siku za Chama katika Jimbo hilo.

**5.8.8.1.2.** Kuwa msemaji na mhamasishaji mkuu wa Chama wa Jimbo.

**5.8.8.1.3.** Kuongoza mikutano ya Jimbo.

**5.8.9. Kazi za Katibu wa Jimbo**

**5.8.9.1.** Kuwa mtendaji na mtunzaji mkuu wa kumbukumbu zote za Chama katika Jimbo.

**5.8.9.2**. Kutunza orodha ya wanachama wote wa Jimbo .

**5.8.9.3**. Kutunza kumbukumbu za mali za Chama zisizoondosheka na zinazoondosheka zilizopo katika Jimbo hilo.

**5.8.9.4.** Kuwa mdhibiti mkuu wa mali za Chama katika Jimbo.

**5.8.9.5**. Kutoa taarifa za kila mwezi za utendaji wa shughuli za Chama katika Jimbo kwa ngazi ya juu.

**5.8.10. Kazi za Mweka Hazina wa Jimbo:**

**5.8.10.1.** Kubuni miradi na kutafuta fedha kwa ajili ya Chama

**5.8.10.2.** Kuweka kumbukumbu za mapato na matumizi ya Chama

**5.8.10**.3. Kuandaa bajeti ya Chama ya Jimbo na kuwasilisha kwenye kamati ya utendaji ya Jimbo pamoja Mkoa.

**5.8.10.4.** Kutoa taarifa ya mapato na matumizi ya Chama.

**5.8.11. Kazi za Afisa habari na taarifa kwa umma wa Jimbo.**

**5.8.11.1.** Kukitangaza Chama ndani na nje ya Jimbo.

**5.8.11.2**. Kukieneza Chama ndani na nje ya Jimbo.

**5.8.11.3**. Ndiye mtoa habari zinazohusu chama kwa umma katika Jimbo.



**5.9. Ngazi ya Mkoa**

**5.9.1.Mkoa utakuwa na vikao vifuatavyo:-**

5.9.1.1 Mkutano wa Mkoa

5.9.1.2 Kamati ya Utendaji ya Mkoa

5.9.1.3 Kamati ya Sekretariati ya Mkoa

**5.9.2. Wajumbe wa Mkutano wa Mkoa:**

**5.9.2.1.** Mwenyekiti wa Mko.

5.9.2.2K atibu wa Mkoa

5.9.2.3Afisa habari na taarifa kwa umma wa Mkoa

5.9.2.4Mweka hazina wa Mkoa.

5.9.2.5Wabunge/Wawakilishi waliochaguliwa/kwa tiketi ya CHAUMMA.

5.9.2.6 Madiwani waliochaguliwa kwa tiketi ya CHAUMMA.

5.9.2.7 Wenyeviti na Makatibu wa Mabaraza katika kila Jimbo

**5.9.2.8.** Wenyeviti na Makatibu wa Chama wa Jimbo.

**5.9.3. Kazi za Mkutano Mkuu wa Mkoa**

5.9.3.1 Kuchagua Mwenyekiti kila unapofika wakati wa uchaguzi

5.9.3.2 Kuchagua Mweka Hazina na Afisa hababari na taarifa kwa Umma wa Mkoa

5.9.3.3 Kupokea taarifa ya Kamati ya Utendaji wa Mkoa na ya Mabaraza ya Chama na kutoa

Maamuzi au mwongozo ama maelekezo kwa utekelezaji.

5.9.3.4 Kumchagua mjumbe mmoja atakayekuwa mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa



5.9.3.5 Kupima utekelezaji wa shughuli za Chama katika Mkoa

5.9.3.6 Kutoa maelekezo yanayofaa kwa ajili ya maendeleo ya chama katika Mkoa

5.9.3.7 Kusilikiliza na kutoa mapendekezo kwa ngazi ya juu kuhusu masuala ya nidhamu kwa wanachama

5.9.3.8 Kuwapatia mwongozo na maelekezo wawakilishi wa Chama walio katika serikali za mitaa

5.9.3.9 Mkutano wa Mkoa utafanyika walau mara moja kwa mwaka.

**5.9.4. Kamati ya Utendaji ya Mkoa**

5.9.4.1.Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Mkoa watakuwa kama ifuatavyo.

**5.9.4.1**.1 Mwenyekiti wa Mkoa

**5.9.**4.1.2.Katibu wa Mkoa

**5.9.**4.1.3.Afisa habari na taarifa kwa umma wa Mkoa

**5.9.**4.1.4.Wenyeviti wote wa mabaraza ya chama wa Mkoa

**5.9.**4.1.5. Wajumbe wawili kutoka kila Jimbo waliochaguliwa na Mkutano wa Jimbo, ambapo mmoja ni mwanamke

**5.9.**4.1.6.Wenyeviti na makatibu makatibu wa majimbo.

**5.**9.4.1.7.Mbunge/Mwakilishi aliyeko ndani ya Jimbo

### 5.9.5. Kazi za Kamati ya Utendaji ya Mkoa:-

5.9.5.1 Kusimamia shughuli za kila siku za Chama.

5.9.5.2 Kuwahimiza wananchi kujiandikisha na kufanya kampeni wakati wa uchaguzi ili kuhakikisha kuwa chama kinapata ushindi

5.9.5.3 Kutafuta wanachama wapya na kuongeza wigo wa kuungwa mkono

5.9.5.4 Kuhakikisha ustawi wa matawi yaliyo katika Kata.

5.9.5.5 Kuwaelekeza wananchi jinsi ya kupata, kutetea na kulinda haki zao na kupinga uonevu unaoweza kufanywa na serikali au kikundi chochote.

*32*

5.9.5.6 Kumjadili aliyeondoka katika chama na ambaye ameomba kurudi katika Chama na Kutoa mapendezo kwa Kamati ya Utendaji ya Jimbo.

5.9.5.7 Kushughulika na nidhamu ya wanachama wa Kata hiyo na kuchukua hatua za nidhamu kwa wanachama

5.9.5.8 Kukieneza Chama katika Kata.

5.9.5.9 Kupokea, kujadili taarifa ya kila mwaka maendeleo ya Kamati ya Utendaji ya Tawi na ya kila baraza la Chama na kutoa maamuzi au mwongozo ama maelekezo kwa utekelezaji.

5.9.5.10 Kusimamia matumizi ya fedha

5.9.5.11 Kumjadili aliyeondoka katika chama na ambaye ameomba kurudi katika Chama na kutoa mapendezo kwa Kamati ya Kata/Wadi

5.9.5.12 Kujadili maombi ya wanaoomba kugombea uongozi wa serikali za mitaa /katika Chama .

5.9.5.13 Kujadili na kupitisha bajeti ya Chama ya Mkoa.

5.9.5.14 Kusimamia matumizi ya fedha

5.9.5.15 Kuwa na mpango mkakati kwa ajili ya kukiimarisha Chama katika Kata

5.9.5.16 Kutekeleza sera na kazi za Chama katika Kata hiyo

5.9.5.17 Kuwaandaa wanachama kushirikiana na wananchi wengine katika kuleta demokrasia ya kweli na maendeleo kwa kushirikiana na vyama vya kijamii.

**5.9.6. Wajumbe wa Sekretariati ya Mkoa**

5.9.6.1. Wajumbe wa Sekretariati ya Mkoa watakuwa kama ifuatavyo:

5.9.6.1.2. Katibu wa Mkoa ndiye mwenyekiti wa Sekretariati

5.9.6.1.3. Afisa habari na taarifa kwa umma wa Mkoa

5.9.6.1.4. Mweka hazina wa Mkoa

5.9.6.1.5 Makatibu watatu WA mabaraza ya wazee, wanawake na vijana wa Mkoa na pia

5.9.6.1.6 Watamchagua katibu wa sekretariati miongoni mwao.

## 5.9.7. Kazi za Sekretariati ya Mkoa.

33

5.9.7.1 Kuandaa dondoo (agenda) na nyaraka za kikao cha Kamati ya Utendaji na mkutano Mkuu

5.9.7.2 Kuandaa bajeti ya Mkoa

5.9.7.3 Utekelezaji wa maamuzi na maelekezo ya kamati ya utendaji

5.9.7.4 Utekelezaji wa kazi za kila siku za uendeshaji wa shughuli za Chama.

**5.9.8. Kazi za Mwenyekiti wa Mkoa**

5.9.8.1 Mwenyekiti wa Mkoa ndiye msimamizi mkuu wa shughuli za kila siku za Chama katika Mkoa.

5.9.8.2 Kuwa msemaji na mhamasishaji mkuu wa Chama wa Mkoa.

5.9.8.3 Kuongoza mikutano yote ya Mkoa kwa mujibu wa Katiba.

**5.9.9. Kazi za Katibu wa Mkoa**

5.9.9.1 Kuwa mtendaji na mtunzaji mkuu kazi za kila siku na kumbukumbu zote za Chama katika Mkoa.

5.9.9.2 Kutunza orodha ya wanachama wote wa Mkoa.

**5.9.9.3.** Kutunza kumbukumbu za mali za Chama zisizoondosheka na zinazoondosheka zilizopo katika Mkoa.

5.9.9.4 .Kuwa mdhibiti mkuu wa mali za Chama katika Mkoa.

5.9.9.5 Kutoa taarifa za kila mwezi za utendaji wa shughuli za Chama katika Mkoa kwa ya Taifa.

**5.9.10. Kazi za Mweka Hazina wa Mkoa**

5.9.10.1. Kubuni miradi na kutafuta fedha kwa ajili ya Chama

5.9.10**.2** .Kuweka kumbukumbu za mapato na matumizi ya Chama

5.9.10**.3**. Kuandaa bajeti ya Chama ya Mkoa na kuwasilisha kwenye kamati ya utendaji ya Mkoa na hatimaye Halmashauri ya Mkoa.

5.9.10**.4.**Kutoa taarifa ya mapato na matumizi ya Chama.

**5.9.11. Kazi za Afisa habari na taarifa kwa umma wa Mkoa.**

**5.9.11.1.** Kukitangaza Chama ndani na nje ya Mkoa.

**5.9.11.2.** Kukieneza Chama ndani na nje ya Mkoa.

**5.9.11.3.** Ndiye mtoa habari zinazohusu chama kwa umma katika Mkoa.

**5.10. Ngazi ya Taifa.**

5.10.1 Kutakuwa na vikao vifuatavyo katika ngazi ya Taifa:

5.10.1.1 Mkutano Mkuu Taifa

5.10.1.2 Halmashauri Kuu Taifa

5.10.1.3 Kamati kuu ya Halmashauri Kuu ya taifa.

5.10.1.4 Sekretariati ya kamati kuu ya Taifa

**5.11 Wajumbe wa Mkutano Mkuu Taifa**

**5.11.1** Mwenyekiti wa taifa



34

**5.11.2** Makamu Mwenyekiti wa Tanzania bara

**5.11.3** Makamu Mwenyekiti wa Tanzania zanzibar

**5.11.4** Katibu mkuu

**5.11.5** Naibu katibu Mkuu Tanzania bara

**5.11.6** Naibu katibu Mkuu Tanzania Zanzibar

**5.11.7** Mweka Hazina

**5.11.8** Afisa habari na taarifa kwa Umma wa Taifa

**5.11.9** Mwenyekiti wa baraza la wadhamini

**5.11.10** Wajumbe wa Halmashauri kuu ya Taifa

**5.11.11** Wenyeviti wa chama wa majimbo, wenyeviti na makatibu wa mikoa.

**5.11.12** Wenyeviti na makatibu wa taifa wa mabaraza

**5.11.13** Rais na Makamu wa Rais wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanaotokana na **Chama**

**5.11.14** Rais na Makamu wa Rais wa serikali ya Mapinduzi Zanzibar anayetokana na Chama.



**5.11.15** Mwenyekiti na Katibuwa Wabunge wanaotokana na Chama.

**5.11.16** Mwenyekiti na Katibu wa Baraza la wawakilishi Zanzibar wanaotokana na chama.

**5.11.17** Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**5.11.18** Makamu wa Rais wa Zanzibar waliotokana na Chama

**5.11.19** Mbunge/Wabunge/Wawakilishi wa Afrika Mashariki waliochaguliwa kupitia Chama

**5.11.20** Wajumbe wa Baraza la wadhamini

**5.12 Kazi za Mkutano Mkuu wa Taifa**

5.12.1 Kuchagua Mwenyekiti wa Chama wa Taifa.

5.12.2 Kuchagua Makamu Mwenyekiti wa Taifa Bara na Makamu Mwenyekiti Taifa Zanzibar.

5.12.3 Kuwachagua wajumbe 10 wa kuwa wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ambao kati yao Wajumbe 7 kutoka Bara na wajumbe 3 watatoka Zanzibar

5.12.4 Kubadilisha/kurekebisha katiba ya Chama.

5.12.5 Kuteua miongoni mwa wanachama mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar

5.12.6 Kupokea na kusikilizaa rufaa kutoka Halmashauri Kuu ya Taifa kwa ajili ya kuthibitishwa au Kubatilishwa au vinginevyo na ndicho kikao chenye maamuzi ya mwisho kwa rufaa zote

5.12.7 Kupokea taarifa zote za kazi za Chama kutoka Halmashauri kuu na kuziridhia au kutoridhia Kazi hizo na au kutoa maelekezo vinginevyo.

5.12.8 Kutoa maelekezo kuhusu utekelezaji wa itikadi, sera na malengo ya Chama

5.12.9 Kumwondoa madarakani kwa mapendekezo ya halmashauri kuu ya Taifa kiongozi yeyote kwa kura zaidi ya nusu ya wajumbe halali walioudhuria

5.12.10 Maamuzi yoyote ya kumuondoa kiongozi yoyote katika nafasi aliyokuwa nayo lazima aridhiwe na Mkutano Mkuu kwa kura za nusu ya wajumbe halali.

36

5.12.11 Kutoa uamuzi wa mwisho juu ya jambo lolote linalohusu chama ambalo ambalo halitajwa katika Katiba hii.

5.12.12 Kupitisha Katiba, ilani na Sera za Chama

5.12.13 Kupanga na kuweka programu za kupata ushindi wakati wa uchaguzi.

5.12.14 Mkutano Mkuu wa Taifa utafanyika kila baada ya miaka mitano (5) isipokuwa kama Kuna suala la dharura mkutano maalum wa taifa unaweza kuitishwa kwa mapendekezo ya Halmashauri Kuu ya Taifa.

## 5.13. Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa

5.13.1 Mwenyekiti wa Taifa.

5.13.2 Makamu Mwenyekiti wa Taifa Bara.

5.13.3 Makamu Mwenyekiti wa Taifa Zanzibar.

5.13.4 Katibu Mkuu.

5.13.5 Naibu Katibu Mkuu Bara.

5.13.6 Naibu Katibu Mkuu Zanzibar.

5.13.7 Mweka Hazina wa chama wa taifa.

5.13.8 Afisa habari na taarifa kwa Umma Taifa

5.13.9 Waweka hazina

5.13.11 Mwenyekiti na Katibu wa Wabunge wa kamati ya Chama

5.13.12 Katibu wa Baraza la wawakilishi Zanzibar Mwenyekiti na Katibu wa Baraza la wawakilishi Zanzibar

5.13.13 Wabunge/Mbunge wa Bunge la jumuiya ya Afirika ya Mashariki waliochaguliwa Kupitia Chama

5.13.14 Raisi na Makamu wa Raisi wajamhuri ya Muungano wa Tanzania waliochaguliwa Kupitia chama

5.13.15 Rais na makamu wa Rais wa serikali ya Mapinduzi Zanzibar waliochaguliwa kupitia chama

5.13.16 Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na waliochaguliwa kupiti Chama

5.13.17 Mjumbe Wajumbe wanne ambapo wawili (2) kutoka bara na wawili (2) kutoka Wajumbe wanawake wanne (4), wawili (2) kutoka Bara na wawili (2 ) kutoka Zanzibar.

5.13.18 Wenyeviti wa Taifa wa Mabaraza ya Chama ya wazee,Wanawake.na vijana.

5.13.19 Wajumbe wawili kuwakilisha makundi maalum mmoja kutoka bara na mmoja kutoka Zanzibar



37

5.13.20 Makamishina wa kanda na Mikoa.

5.13.21 Mwenyekiti na katibu wawakilishi waliochaguliwa kwa tiketi ya chama cha Ukombozi wa umma (CHAUMMA)

5.14 **Kazi za Halmashauri Kuu Taifa**

5.14.1 Kusimamia utekelezaji wa sera za Chama.

5.14.2 Kumchagua Katibu Mkuu,na Manaibu wake wote Tanzania Bara na Zanzibar.

5.14.3 Kuwahimiza wananchi kujiandikisha na kufanya kampeni wakati wa Uchaguzi ili kuhakikisha kuwa chama kinapata ushindi.

5.14.4 Kutafuta wanachama wapya na kuongeza wigo wa kuungwa mkono na Wanachama na wananchi kwa ujumla.

5.14.5 Kuhakikisha ustawi wa Mikoa

5.14.6 Kujadili maombi ya wanaoomba kugombea uongozi wa umeya, ubunge na ya Uongozi katika Chama ngazi ya Mkoa, Kanda na Taifa na kuyatolea uamuzi. 38

5.14.7 Kumjadili aliyeondoka katika chama na ambaye ameomba kurudi katika Chama na kutoa mapendekezo

5.14.8 Kuongoza katika harakati za kupinga uonevu unaoweza kufanywa na serikali au kikundi chochote na kuwaelimisha wananchi na kuwatetea ili kulinda haki zao.

5.14.9 Kuwaelekeza wananchi jinsi ya kupata, kutetea na kulinda haki zao

5.14.10 Kushughulika na nidhamu ya viongozi na wanachama na kuchukua za kinidhamu kwa wanachama

5.14.11 Kujadili maombi ya wanaoomba kugombea uongozi wa umeya, ubunge na uongozi katika Chama ngazi ya wilaya , Mkoa,Kanda na Taifa na kuyatolea maamuzi.

5.14.12 Kujadili na kupitisha bajeti ya Chama ya Taifa

5.14.13 Kupokea, kujadili na kupitisha taarifa ya kila mwaka ya maendeleo ya kila baraza la Chama.Kukieneza Chama na kutekeleza sera za Chama katika nchi

5.14.14 Kuwa na mpango mkakati kwa ajili ya kukiimarisha Chama Kitaifa

5.14.15 Kuteua Mwenyekiti na wajumbe wa Baraza la wadhamini la Chama na kumuondoa kwenye baraza la wadhamini baada ya kupewa nafasi ya kujieleza na kujitetea .

5.14.16 Halmashauri Kuu Taifa itakutana angalau mara mbili kwa mwaka

5.14.17 Itateua au kutengua makatibu wa chama ngazi ya mkoa na majimbo kama itakavyopendekezwa na kamati kuu.

5.14.18 Kumteua na kutengua uteuzi wa Katibu Mkuu na Wajumbe wa sekretarieti utafanywa na Mwenyekiti waTaifa kupitia kamati kuu ya Halmashauri kuu ya Taifa.



5.14.19 Kumchagua Mweka hazina na Afisa habari na Taarifa kwa umma.

## 5.15 Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu

5.15.1.Wajumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa watakuwa kama ifuatavyo:-

5.15.1.1 Mwenyekiti wa Taifa

5.15.1.2 Makamu Mwenyekiti Bara

5.15.1.3 Makamu Mwenyekiti Zanzibar

5.15.1.4 Katibu Mkuu

5.15.1.5 Naibu Katibu Mkuu Bara

5.15.1.6 Naibu Katibu Mkuu Zanzibar.

5.15.1.7 Mweka Hazina Taifa.

5.15.1.8 Afisa habari na taarifa kwa Umma Taifa.

5.15.1.9 Wenyeviti wa Taifa wa Mabaraza ya Wanawake, Wazee na

Vijana.

5.15.1.10Mwenyekiti wa kamati ya Wabunge wanaotokana na Chama.

5.15.1.11Mwenyekiti na katibu wa wenyeviti wa mikoa wa chama.

5.15.1.12 Wajumbe wa Sekretarieti-Waalikwa

5.15.1.13Wajumbe watatu (3) watateuliwa na Mwenyekiti

5.15.1.14Mwenyekiti wa Baraza la wadhamini

**5.16 Kazi za Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa.**

5.16.1 Kusimamia shughuli za kila siku za Chama.

5.16.2 Kuwahimiza wananchi kujiandikisha, kufanya kampeni na kuhakikisha kuwa chama kinapata ushindi.

5.16.3 Kutafuta wanachama wapya

5.16.4 Kusimamia ustawi wa chama katika nchi

5.16.5 Kuhakikisha kwamba wakati wa uchaguzi kampeni zinafanywa kwa lengo la kukipatia chama ushindi.

5.16.6 Kujadili na kupitisha uamuzi juu ya maombi ya waliojiuzulu au kutoa mapendekezokwa Kamati Tendaji ya Jimbo kwa walio jiuzulu na kujiunga tena na Chama.

5.16.7 Kuongoza harakati za kupinga uonevu unaoweza kufanywa na serikali au kikundi chochote

5.16.8 Kuchagua wakurugenzi wa idara Makao Makuu ya Chama.

5.16.9 Kushughulika na nidhamu ya viongozi na wanachama katika mkoa na kuchukua hatua za Kinidhamu.

5.16.10Kumjadili aliyeondoka katika chama na ambaye ameomba kurudi katika Chama na kutoa uamuzi.

5.16.11Kujadili na kutoa mapendekezo ya maombi ya wanaoomba kugombea

*40*

uongozi ndani ya Chama na uongozi wa serikali kwa maamuzi.

5.16.12 Kujadili na kupitisha bajeti ya Chama

5.16.13 Kupokea, kujadili na kupitisha taarifa ya kila mwaka ya maendeleo ya kila baraza la Chama.

5.16.14 Kukieneza Chama katika nchi

5.16.15 Kutekeleza sera na kazi za Chama katika nchi

5.16.16 Kupanga ratiba na mikakati ya kupata raslimali kwa ajili ya uchaguzi.

5.16.17 Kutekeleza sera na kazi za Chama katika nchi.

5.16.18 Kujadili na kupendekeza wagombea wa uwakilishi ngazi ya jimbo na Taifa.

5.16.19 Kuwaandaa wanachama kushirikiana na wananchi wengine katika kuleta demokrasia ya kweli na maendeleo kwa kushirikiana na vyama vya kijamii.

5.16.20 Kuandaa na kutoa mapendekezo kwa Halmashauri kuhusu programu za Chama

41

5.16.21 Kupendekeza ratiba za chama kwenye vikao vya Halmashauri Kuu

5.16.22 Kutoa mwongozo wa siasa kwa taifa.

5.16.23 Kupendekeza wagombea katika Chama kuanzia ngazi ya Jimbo mpaka Taifa.

5.16.24 Kuandaa mkutano wa Halmashauri Kuu ya Taifa

5.16.25 Kufanya utafiti wa wagombea ngazi zote za uchanguzi

5.16.26 Itafanya kazi yake kwa maelekezo ya Halmashauri Kuu ya Taifa

5.16.27 Kuteua kamati maalumu ya kusimamia masuala maalumu ya Chama na yasiyokuwa ya Chama

5.16.28 Kusimamia utekelezaji na utendaji wa mabaraza ngazi ya Taifa

5.16.29 Kusimamia utendaji wa wawakilishi kupitia Chama

5.16.30 Itasimamia kazi za Sekretariati Kuu ya Chama Taifa na kufanya maamuzi ya kiutendaji.

5.16.31 Kamati Kuu Taifa itapendekeza majina yasiyopungua sita na yasiyozidi kumi kati yao moja ya tatu wawe wanawake. Wajumbe hao watathibitishwa na Halmashauri Kuu Taifa kuwa wajumbe wa Baraza la Wadhamini baada kupata baraka za Mkutano Mkuu Taifa.

5.16.32 Kamati Kuu ya Chama itakutana walau mara nne (4) kwa mwaka

## 5.17. Sekretariati ya Kamati Kuu

5.17.1 Wajumbe wa Sekretariati ya Kamati Kuu ni kama ifuatavyo :-

5.17.1.1.1 Katibu Mkuu

5.17.2 Naibu Katibu Mkuu Bara

5.17.3 Naibu Katibu Mkuu Zanzibar

5.17.4 Wakurugenzi wa Idara zote

5.17.5 Afisa habari na taarifa kwa Umma Taifa

5.17.6 Wajumbe wanane wataalam watakaoteuliwa na Mwenyekiti kwa Kushauriana na Ofisi ya Katibu Mkuu

5.17.7 Makatibu watatu wa Mabaraza ya Chama Taifa na pia watachagua Miongoni mwao atakayekuwa Katibu Mkuu wa Sekretariati.

**5.18. Kazi za Sekretariati ya Kamati Kuu ya Taifa.**

5.18.1 Utekelezaji wa kazi za kila siku za uendeshaji wa shughuli za Chama

5.18.2 Kuandaa dondoo (agenda) na nyaraka za kikao cha Kamati Kuu.

5.18.3 Kuandaa bajeti kwa ajili ya kuiwakilisha kwenye Kamati Kuu na Halmashauri Kuu

5.18.4 Kutekeleza maamuzi na maelekezo ya Kamati Kuu.



*42*

5.19 **Idara za Sekretariati ya Chama**

5.19.1 Kutakuwa na Sekretariati ya Chama katika kila ngazi; za Tawi ,Kata/Wadi, Jimbo,Mkoa na Taifa.

5.19.2 Katika ngazi ya Taifa kutakuwa na Sekretariati katika Makao Makuu ya Chama DaresSalaam na katika ofisi ndogo ya Makao Makuu Zanziba.

**5.20 Sekretarieti ya kila ngazi itakuwa na idara zifuatazo:-**

5.20.1 Idara ya Uchumi na Fedha na mipango

5.20.2 Idara ya Habari na Taarifa kwa Umma

5.20.3 **Idara** ya Uchaguzi, Kampeni na Oganaizesheni

5.20.4. Idara ya Ulinzi na Usalama.

5.20.5. Idara ya Mahusiano na Mambo ya Nje na ushirikiano wa kimataifa.

43

5.21 Idara ya Itikadi, mafunzo na elimu kwa Umma

5.20.6 Idara ya viongozi wa wakilishi wa wananchi kupitia Chama.

5.20.7 Idara ya Sheria, Katiba, Haki za binadamu na Maendeleo ya jamii

5.20.8 Katibu wa Chama atakuwa Mwenyekiti wa Sekretarieti ya ngazi yake.

5.20.9 **.** Itafanya kikao walau mara moja kila mwezi.

# SURA YA SITA

## 6. MUUNDO WA NGOME ZA CHAMA

6.1.Chama kitakuwa na ngome zifuatazo:

6.1.1 Ngome ya Wazee

6.1.2 **Ngome** ya Wanawake

6.1.3 Ngome ya Vijana

6.1.4 Ngome zote za Chama yatakuwa chini ya Uongozi wa Chama wa ngazi husika na zitawajibika kwa ngazi hiyo kupitia kwa Katibu wa Chama wa ngazi hiyo.

## 6.2. MASHARTI YA KUWA MWANACHAMA WA KILA NGOME.

6.2.1. Mwanachama atakuwa ni mwanachama wa Ngome mojawapo kwa masharti kama ifuatavyo:-

6.2.1.1 Uanachama wa Ngome ya vijana ni mwanachama wa Chaumma aliye na umri wa kupiga kura hadi miaka 35.

6.2.1.2 Uanachama wa Ngome ya wazee na ya wanawake ni miaka 36 na kuendeleala vijana ni mwanachama wa Chaumma aliye na umri kupiga kura hadi miaka 35.

*44*

## 6.3. KANUNI ZA KUENDESHA NGOME NA UCHAGUZI NDANI YA MABARAZA

6.3.1 Kila ngome itatunga kanuni za kusimamia uendeshaji wa shughuli zake na kanuni hizo

6.3.2 Zitaanza kutumika baada ya kupitishwa na Halmashauri Kuu ya Taifa.

6.3.3 Majina ya wagombea kiti cha Mwenyekiti wa kila Ngome wa Tawi au Kata/Wadi au Jimbo, Mkoa na Taifa yatajadiliwa na kupitishwa na kikao cha utendaji cha Chama katika ngazi husika.

6.3.4 Kila Ngome inatoa taarifa ya maendeleo ya kazi zake kila baada ya miezi mine(4) kwa Kamati ya Utendaji ngazi husika, lakini Ngome za Taifa zitatoa taarifa zake kwa Kamati

Kuu ya Taifa.

## 7 SURA YA SABA

## 7. BARAZA LA WADHAMINI LA CHAMA

Kutakuwa na Baraza la Wadhamini la Chama lenye wajumbe wafuatao:

**7.1.** Mwenyekiti wa Baraza

**7.2.** Katibu wa Baraza

**7.3**. Wajumbe sita; wakiwamo walau wanawake wawili.

**7.4. Majukumu ya Baraza la Wadhamini.**

**7.4.1.** Baraza litakuwa na mamlaka na uwezo wa kuyatumia mamlaka yake kama ilivyopewa na sheria ya wadhamini.

45

**7.4.2**. Baraza litafanya kazi zake chini ya usimamizi na maelekezo ya Halmashauri Kuu ya Taifa na litatoa taarifa ya shughuli zake Halmashauri Kuu ya Taifa.

**7.4.3**. Kuweka chini ya uangalizi wake mali zote za Chama zinazoondosheka na Zilizoondosheka.

**7.4.4**. Kuingia katika shughuli zozote za uchumi ambazo zinaendana na madhumuni na malengo ya chama kwa kibali cha Halmashauri Kuu ya Taifa.

**7.4.5**. Kutoa taarifa ya utendaji ya mwaka katika kikao cha Halmashauri Kuu ya Taifa.

7.4.6. Bila ya kuathiri masharti ya Sheria na kanuni za Baraza la Wadhamini, Baraza linaweza Kuitisha mkutano maalum pale itakapolazimu kufanya hivyo.

**7.4.7**. Mdhamini atakuwa kwenye nafasi ya udhamini kwa muda wa miaka mitano (5) ya kwanza na anaweza kuteuliwa kuendelea na nafasi hiyo baada ya kipindi chake kumalizika kwa mara ya pili na ndiyo kitakuwa kipindi chake cha mwisho.

**7.4.8**. Baraza litafanya kikao mara moja katika kila baada ya miezi mitatu (3).

**7.5. Mjumbe wa Baraza la Wadhamini ataondolewa katika uongozi na Halmashauri Kuu ya Taif a ikiwa:-**

**7.5.1**. Ana afya mbaya kiasi cha kushindwa kufanya kazi zake.

**7.5.2.** Ameishi nje ya nchi kwa miaka miwili mfululizo.

**7.5.3**. Ikiwa atakuwa amekiuka katiba na maadili ya Chama.

**7.5.4**. Ikiwa atapatikana na hatia ya kosa ambalo Halmashauri Kuu ya Taifa itaridhika kuwa Kulingana na uzito wa kosa halikustahili kufanywa na mdhamini wa Chama

**7.5.5.** Mdhamini atajiuzulu kutoka katika Baraza kwa kutoa tamko la maandishi kwa Halmashauri Kuu ya Taifa kupitia kwa Mwenyekiti wa Baraza.

**7.5.6.** Iwapo itatokea nafasi wazi kutokana na kifo, kujiuzulu au kupumzishwa kwa mdhamini, nafasi Hiyo itajazwa mara moja kwa kumchagua kwa kura mwanachama mwingine kufuatana kufatana nataratibu za katiba hii

**7.5.7.** Iwapo Mwenyekiti wa Baraza atashindwa kuhudhuria vikao, wajumbe watamchagua mmojawapo kati yao kuwa Mwenyekiti wa kikao cha siku hiyo.



**SURA YA NANE 8**

**8. VIONGOZI WAKUU WA CHAMA NA KAZI ZAO**

Viongozi Wakuu wa Chama watakuwa:

**8.1**. Mwenyekiti wa Taifa.

**8.2**. Makamu Mwenyekiti wa Taifa Bara.

**8.3.** Makamu Mwenyekiti wa Taifa Zanzibar.

**8.4.** Katibu Mkuu Taifa.

**8.5**. Naibu Katibu Mkuu Taifa Bara.

**8.6.** Naibu Katibu Mkuu Zanzibar

**8.7.** Afisa habari na Taarifa kwa Umma

**8.8.** Mkurugenzi wa FedhaTaifa.

**8.9. Mwenyekiti wa Taifa:**

**8.9**.1. Atakuwa kiongozi mkuu wa Chama na atakuwa msemaji mkuu wa Chama.

**8.9.2.** Atakuwa ndiye mhamasishaji mkuu wa Chama

**8.9.3**. Atakuwa Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu wa Taifa na Halmashauri Kuu ya Taifa na Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa

8.9.4**.** Atakuwa Mwakilishi Mkuu katika matukio ya kitaifa akiwepo nchini au kuwakilishwa.

**8.9.5**. Atakuwa Mkuu wa Chuo cha Chama

**8.9.6.** Atakuwa katika nafasi hiyo kwa muda wa miaka mitano (5) na anaweza kuchaguliwa tena kila baada ya miaka mitano (5).



8.9.7. Atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa nafasi zote za uongozi zilizo wazi kwa namna yoyote zina jazwa kwa njia ya uchaguzi ndani ya chama na kwa mujibu wa katiba hii.

8.9.8. Ataweza kuondolewa katika uongozi baada ya mapendekezo ya Halmashauri Kuu ya Taifa kwa azimio la Mkutano Mkuu Maalumu wa Taifa litakaloungwa mkono na theruthi mbili ya kura za wajumbe

halali waliohudhuria na kupiga kura.

8.9.9.Katika mikutano anayoiongoza mwenyekiti hatapiga kura katika kura ya maamuzi,lakini Mwenyekiti atalazimika kupiga kura endapo kura za Wajumbe wanaoafiki na wasioafiki zitalingana.

**8.9.10.** Atateua wajumbe wanane wataalam watakaokuwa wajumbe wa Sekretariati ya Kamati Kuu ya Taifa

8.9.11.Iwapo Mwenyekiti wa Taifa hayupo kwa sababu yoyote ya kikazi au ya kiafya,Makamu Mwenyekiti wa Taifa atakaimu uenyekiti wa Chama wa Taifa .

8.9.12.Iwapo kiti cha Mwenyekiti wa Taifa kitakuwa wazi kwa kuwa nje ya nchi kwa sababu yoyote ile utaratibu ufuatao utatumika.

8.9.13. Makamu mweyekiti wa chama Zanzibar atakaimu kwa kipindi cha kwanza cha miezi mitatu (3) na Makamu mwenyekitiwa chama Bara atakaimu kwa kipindi cha pili cha miezi mitatu (3)

8.9.14.Iwapo nafasi ya mwenyekiti wa taifa itakuwa wazi kwa sababu za kujiuzulu ,kuondoka katika chama ,kuvuliwa uongozi,au maradhi yenye kuondoa uwezo wa kufanya kazi au kifo . Mkutano Mkuu maalum wa Taifa utaitishwa katika muda usiozidi miezi sita tangu kuwa wazi kwa kiti hicho; ili kumchagua Mwenyekiti wa Taifa mwingine.

8.10**. Makamu Wenyeviti wa Taifa**

**8.10.1**.Makamu Wenyeviti wa Taifa watakuwa ndio wasaidizi wakuu wa Mwenyekiti Taifa na mmoja kati yao ndiye atakaye kaimu wakati Mwenyekiti wa Taifa hayupo .

**8.10.2**. Wataweza kuachishwa kwenye uongozi baada ya mapendekezo ya Halmashauri Kuu ya Taifa kwa azimio la Mkutano Mkuu wa Taifa litakaloungwa mkono na theruthi mbili ya kura za wajumbe halali waliohudhuria na kupiga kura.

48

**8.10.2.** Makamu watahusika zaidi na shughuli za uhamasishaji na kampeni za Chama na majukumu Mengine watakayopewa na Mwenyekiti wa Chama Taifa.

**8.10.2**. Makamu mwenyekiti Zanzibar atakapokuwa hayupo nchini naibu Katibu mkuu Zanzibar atakaimu nafasi hiyo.

**8.11. Katibu Mkuu**

8.11.1. Atakuwa Mtendaji Mkuu wa Chama

8.11.2. Atakuwa Katibu wa vikao vya Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa, Halmashauri Kuu ya Taifa na Mkutano Mkuu wa Taifa

8.11.3. Atakuwa Katibu wa Baraza la Wadhamini

8.11.4. Atakuwa Mwenyekiti wa Sekretarieti ya Taifa

8.11.5. Atakuwa na mamlaka ya kuajiri kufukuza na kusimamia nidhamu ya watumishi

wote wa chama kwa mujibu wa katiba, kanuni taratibu za chama na sheria za nchi

8.11.6. Atafanya kazi yoyote itakayokuwa imetajwa penginepo katika katiba hii.

**8.12. Naibu Makatibu Wakuu**

**8.12.1.** Watamsaidia Katibu Mkuu na kukaimu kiti chake wakati Katibu Mkuu akiwa hayupo,

**8.12.2**. Naibu katibu mkuu bara atafanya kazi zake zaidi Tanzania Bara na Naibu katibu mkuu Zanzibar Atafanya kazi zake zaidi Tanzania Zanzibar.

**8.12.3.** Watafanya kazi nyingine zozote za Chama watakazopewa na Halmashauri kuu ya Taifa.

8.12.4. Watafanya kazi zozote zitakazokuwa zimetajwa penginepo katika katiba hii.

**8.13. Muweka hazina wa chama wa taifa.**

8.13.1. Atadhibiti mapato na matumizi ya fedha za Chama.

8.13.2. Ataandaa bajeti ya Chama

8.13.3. Viongozi wote wa Zanzibar watapendekezwa na wazanzibari wenyewe na mapendekezo haya kwa hali yoyote yaheshimiwe.

49

**SURA YA TISA. 9**

**9. WAGOMBEA URAIS**

**9.1.Masharti kuhusu Mgombea Urais:**

9.1.1. Awe anakidhi masharti ya katiba ya nchi kuhusu mgombea wa kiti cha urais.

**9.1.2**. Awe tayari ni mwanachama wa CHAMA CHA UKOMBOZI WA UMMA .(CHAUMMA) , aliyetimiza sifa za kuwa kiongozi na awe amejihusisha katika uongozi wa aina yoyote Katika jamii.

**9.1.3**. Awe anaelewa katiba na sera za Chama.

**9.1.4.** Atapendekeza jina la mgombea mwenza kwa Halmashauri Kuu ya Taifa ambayo ikiridhia atakuwa mgombea mwenza wakati wa kugombea urais.

**9.1.5**. Iwapo mgombea urais atashinda, atakuwa ndiye mtunzaji na msimamizi wa sera za chama na serikali.

9.1.6. Masharti haya yanamhusu pia mgombea urais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

## SURA YA KUMI

## 10 MAMBO YA JUMLA KUHUSU CHAMA

## 10. MAMBO YA JUMLA NA MUHIMU KUHUSU CHAMA.

### 10.1. Uchaguzi

10.1.1. Uchaguzi Mkuu wa viongozi wa Chama utafanyika kila baada ya miaka mitano (5) au vinginevyo kwa azimio la Mkutano Mkuu wa chama wa Taifa

10.1.2. Katika uchaguzi kila ngazi ya uongozi kuanzia Chemchemi hadi Jimbo itasimamiwa na ngazi ya juu yake na ngazi ya Taifa itasimamiwa na utaratibu utakaowekwa na Halmashauri Kuu ya Taifa .

50

10.1.3. Kiongozi wa ngazi ya Taifa aliyekwisha tumikia nafasi ya chama miaka kumi mfululizo haruhusiwi kugombea tena nafasi hiyo aliyokuwa nayo badala yake anaweza kugombea nafasi nyingine yoyote ya chini yake.

10.1.4.Ili kujaza nafasi iliyoachwa wazi kutokana na aliyekuwa ameshikilia nafasi hiyo

Kujiuzulu, kuachishwa uongzi ama kufariki dunia kwa mujibu wa katiba hii, Uchaguzi unaweza kufanyika wakati wowote bila kungoja kipindi cha miaka mitano cha uongozi uliopo katika Chama kupita.

10.1.5. Viongozi wote wakuchaguliwa kutoka Zanzibar watapendekezwa na Wazanzibari wenyewe

10.1.6.Ili kuepuka chuki na kutoa uhuru zaidi kwa wapiga kura, uchaguzi wa aina yoyote ndani ya Chama ngazi zote utakuwa kwa kura za siri tu.

10.1.7. Wakati wa mkutano wa uchaguzi, mwanachama ambaye siyo mgombea

atachaguliwa na wajumbe kuongoza mkutano huo wa uchaguzi.

**10.2. RUZUKU NA MAPATO MENGINE YA CHAMA.**

Ruzuku zita gawanywa kama ifuatavyo,

10.2.1. Makao makuu ya chama itapata asilimia sabini 70%.

10.2.2. Ofisi ndogo ya chama Zanzibar itapata asilimia thelathini 30%.

**10.3. AKIDI YA KILA KIKAO CHA CHAMA;**

Akidi ya kila kikao cha Chama itakuwa nusu ya wajumbe halali wa kikao hicho.

## 10.4. Uitishaji wa vikao:

10.4.1. Vikao vyote vya chama vitaitishwa na Mwenyekiti kwa kumuagiza katibu wa ngazi husika

10.4.2. Vikao vya mikutano mikuu ya Taifa na Jimbo vya kawaida vitaitishwa kwa taarifa ya siku zisizopungua ishirini na moja (21) Na kwa vyovyote iwavyo kikao chochote Kitaitishwa kwa taarifa ya maandishi tu na si kwa kutumia ujumbe mfupi au barua pepe.

51

10.4.3. Vikao vya kawaida vya Halmashauri Kuu ya Taifa, Kamati Kuu ya Taifa, Kamati ya Jimbo,Kata/ Wadi na Mkutano Mkuu wa Tawi vitaitishwa kwa taarifa ya siku zisizopangua kumi na nane ( 18)

10.4.4.Vikao vya kawaida vya Kamati ya Tawi na Mkutano wa Chemchemi vitaitishwa kwa taarifa ya siku zisizopungua kumi (10) na pia kutakuwepo na vikao maalum au vya dharura vinavyoweza kuitishwa wakati wowote kwa taarifa ya dharura .

10.4.5. Muda wa taarifa ya kuitisha kikao chochote kilichotajwa katiba hii unaweza kuwa pungufu

ya muda uliotajwa iwapo kikao kinachoitishwa ni maalum au dhararu ,wajumbe watapewa taarifa ya maandishi si chini ya muda wa siku kumi na mbili ( 12)

10.4.6 Kwa vikao vya kawaida Mwenyekiti atawajibika kuwaeleza wajumbe kwanini kikao

hakifanyiki na atatoa tarehe ya kufanyika kwa kikao husika na katibu atawajulisha wajumbe

**10.5. Mjumbe wa kikao kupoteza sifa:**

ambaye hatahudhuria vikao vitatu mfululizo bila taarifa na sababu za kutofika kwa uongozi unaohusika na kikao husika au sababu inayokubalika atakuwa amejivua ujumbe katika kikao hicho.

**10.6. Ratiba ya Vikao:**

10.7.Kila kikao cha Chama kitafanyika katika muda uliotajwa katika katiba hii isipokuwa likitokea jambo maalum au la dharura lililotajwa katika katiba hii linalohitaji kikao kifanyike.

**10.8.Kukasimu Mamlaka na Madaraka.**

10.8.1.Kikao chochote cha chama kinaweza kukasimu madaraka kwa azimio la kikao kilicho chini yake .

10.8.2.Katika kufanikisha shughuli zake kikao chochote cha Chama kinaweza kuunda kamati au tume kwa ajili hiyo na kamati au tume hiyo itapewa hadidu za rejea na kikao hicho na kuwajibika kwa kikao hicho



**10.9. KUKAIMU MADARAKA.**

10.9.1. Endapo nafasi itakuwa wazi kwa sababu zozote zinazokubalika kikatiba kikao husika kitakaimisha nafasi hiyo kwa mwanachama mwenye sifa.

10.9.2. Muda wa kukaimu nafasi yoyote utakoma pindi aliyekaimiwa kurudi katika nafasi yake au Mwanachama mwingine kuchaguliwa kushika nafasi hiyo na kwa vyovyote muda wa kukaimu hautozidi miezi sita (6) labda kwa maelekezo ya halmashauri kuu ya taifa

**10.10. Kura za uamuzi:**

10.10.1. Uamuzi wowote utafikiwa kwa kuungwa mkono na zaidi ya nusu ya kura zote za Wajumbe halali waliohudhuria kikao.

10.10.2. Mwenyekiti wa kikao hatapiga kura ya uamuzi, lakini atalazimika kupiga kura iwapo kura zinazoafiki na zisizoafiki zinalingana**.**

**10.11.** KAMATI **YA NIDHAMU, USULUHISHI NA MAONYO :**

Kila itakapohitajika, Kamati ya Nidhamu na Usuluhishi yenye wajumbe watano itaundwa na kila kikao cha Chama cha kiutendaji cha kila ngazi kuanzia Chemchemi Tawi hadi Taifa na itaendesha shughuli zake kwa mujibu wa kanuni za nidhamu na usuluhishi zitakazowekwa na Halmashauri Kuu ya Taifa. Kamati hii itashughulikia nidhamu ya viongozi wakuchaguliwa na wanachama na watumishi wa kuajiriwa watasimamiwa na sheria za kazi za nchi, na kanuni za utendaji au ajira zitakazowekwa na Halmashauri Kuu ya Taifa.

**10.12. TAASISI, ASASI NA NISHANI ZA CHAMA:**

**10.12.1**. Halmashauri Kuu ya Taifa itakuwa na mamlaka ya kuunda taasisi na asasi kwa kadri itakavyoona inafaa kwa maslahi na maendeleo ya Chama ambazo zitakuwa zinajiendesha zenyewe.

**10.12.2.** Pasipo kukiuka Katiba ya Chama Halmashauri Kuu ya Taifa itakuwa na mamlaka ya kuunda nafasi yeyote na kutoa Nishani yoyote katika utekelezaji wamalengo madhumuni ,sera na itikadi ya Chama

**10.13. MABADILIKO /MAREKEBISHO YA KATIBA:**



10.13.1. Katiba inaweza kubadilishwa au kurekebishwa na Mkutano Mkuu wa Taifa kutokana na mapendekezo ya Halmashauri Kuu ya Taifa.

10.13.2.Mabadiliko au marekebisho yoyote ya Katiba hii yatafanyika kwa akidi ya mahudhurio isiyo zaidi ya nusu ya wajumbe halali wa Mkutano Mkuu wa Taifa.

10.13.3. Mabadiliko au marekebisho ya Katiba yatakuwa halali kama yatafanywa na kukubaliwa na nusu ya wajumbe halali waliohudhuria na kupiga kura.

10.14. **CHAMA KUUNGANA NA CHAMA KINGINE/VYAMA VINGINE VYA SIASA.**

10.14.1. Chama kinaweza kuungana na Chama kingine/ Vyama vingine vya siasa kwa kupoteza jina lake la awali kwa azimio la Mkutano Mkuu wa Taifa.

**10.14.2.** Chama kinaweza kushirikiana na Chama kingine/ vyama vingine vya siasa kwa azimio la Halmashauri kuu ya Taifa.

**MWISHO**

54